# KOZI YA KUIJUA BIBLIA

## AGANO LA KALE

## SEHEMU YA II

### Vipo wapi?

*(Uchapaji wa kitabu hiki kwa ajili ya matumizi ya binafsi au kanisa unaruhusiwa. Kunakili kwa aina nyingine, kama kwa ajili ya usambazaji, kwa makusudi ya kutangaza, au kuuza, hairuhusiwi.)*

**Kuijua Biblia, Sehemu ya II Agano la Kale**

By Rosemary P. Nelsen
540 Fairview Avenue, Ripon, WI 54971
rosemarypricenelsen@gmail.com

Bachelor of Science: Education
University of Wisconsin, Oshkosh, WI. Spring, 1972

Elementary Teacher, Washburn, WI, 1972-1977

14 graduate credits from Columbia Graduate School of Bible and Missions, Columbia, S.C., Fall, 1977

Newspaper Reporter/Bureau Chief, Oshkosh Northwestern
Berlin and Ripon Bureaus, 1978-1996

Majukumu mbali mbali ya kazi katika Kanisa ikiwa pamoja na Mwenyekiti wa Elimu ya Kikristo, Mwenyekiti wa Huduma ya wanawake, Mwenyekiti wa Maombi na mara kwa mara Kiongozi wa Masomo ya Biblia, Mwalimu wa Shule ya Jumapili nk.
Kwa kipindi cha cha 1972 mpaka wakati wa sasa

---

**Kimehaririwa na**

Lois E. Gloyd
421 E. Jackson Street, Ripon, WI 54971
legloyd@gmail.com

Associate Degree: Computer Technology 1991
Moraine Park Technical College
Fond du Lac, WI

Aliajiriwa katika Lutheran Homes za Oshkosh 1991 – 2015

Alishakuwa na machapisho katika:
*Country* Magazine
Feb/March 1999
*GreenPrints* Magazine
Spring 2005 and Autumn 2013
*Upper Room* Devotional Guide
July/Aug 2002 and March/April 2010

Mwanzilishi mwenza wa **Sweeter than Honey Ministries** mwaka 2012
Misheni yetu ni kufundisha mambo ya msingi ya Biblia pamoja na Neno Lake, ambalo litahamasisha ukuaji katika Biblia kwa njia ya "kufanywa upya nia zetu" ambako kutatuongoza katika kupima na kuthibitisha "mapenzi ya Mungu yaliyo makamilifu" katika maisha yetu.
*"Mausia yako ni matamu sana kwangu, Kupita asali kinywani mwangu."*
*Zab. 119:103 NIV*

# Agano la Kale Sehemu ya II

*Kusudi kuu la kozi hii ni kuelewa kwamba vitabu 22 vya mwisho vinaongeza maarifa ya kihistoria ya kipindi ambacho vilikuwapo.*

## VIPO WAPI?

Ni wapi ambapo vitabu vya mwisho 22 vya Agano la Kale
vipo katika vile vipindi nane vya historia?

Vitabu 5 vya Sheria
Vitabu 12 vya Historia
Vitabu 5 vya Mashairi
Manabii Wakuu 5
Manabii Wadogo 12

## KUPITIA VIPINDI VYA HISTORIA

1. Enzi ya Mwanzo (Mwanzo 1-11)
2. Mababa (Mwanzo 12-50)
3. Israeli Inakuwa Taifa (Kutoka-Kumbukumbu la Torati)
4. Ushindi na Kumiliki nchi (Yoshua, Waamuzi, Ruthu)
5. Ufalme Mmoja (I Samweli hadi II Wafalme 11)
6. Ufalme uliogawanyika, ikiwa ni pamoja na Yuda peke yake (II Wafalme 12 hadi II Mambo ya Nyakati)
7. Kipindi cha Uhamisho (Yoeli, Obadia, Ezekieli, Danieli)
8. Kipindi Baada ya Uhamisho (Ezra, Nehemia, Esta)

*Maoni kwa mwalimu: Wakati haya yakifundishwa na mwandishi, anafanya hivi kwa mtindo wa kimazungumzo. Chini ya kila kitabu kuna taarifa nyingi kuhusu kitabu hicho na kipo wapi katika makundi nane ya historia ya Agano la Kale. Anasema inaweza kuwa taarifa yenye mambo mengi yanayoweza kusababisha uwasilishaji kukwama ikiwa utajaribu kutumia mengi zaidi na kupitiliza. Inaweza kuwa vizuri zaidi kuwapa picha ya haraka ili kuamsha hamu ya wanafunzi ya kupokea maarifa yatakayowachochea. Kisha ndipo wanaweza kurudi na kujifunza wenyewe kile kinachotolewa hapa, au kujifunza kuhusu kitabu mahali pengine. Mwanzoni mwa baadhi ya vitabu, mwandishi ameweka baadhi ya yale anayoyasema wakati anapokiwasilisha. Hata hivyo, unaweza kufanya kile unachopenda kilicho kweli kuhusiana na kitabu. Mungu akubariki unapoifundisha kozi hii. Inahitajika sana, hasa kwa sababu inatoa uelewa wa historia katika mambo mengine yanayotokea katika wakati wa historia ya Agano la Kale.*

# VITABU VYA MASHAIRI –

# AYUBU (SURA 42)

**Muhtasari wa maelezo: Mungu alimruhusu shetani kumjaribu Ayubu kupitia kuipoteza familia na afya. Aliumizwa pia na marafiki kwa muda ambao walifikiri kwamba ametenda dhambi. Ayubu alikuwa mshindi, lakini soma kitabu kugundua ilikuwaje.**

Ayubu anaweza kuwa ni wa kipindi kile cha Ibrahimu, lakini zaidi sana wa kipindi cha Musa kwa kuwa Edomu ilikuwa ni nchi ya uzao wa Esau. Baada ya majaribu makubwa kwa sababu ya changamoto ya Shetani kwa Mungu, Ayubu anathibitika kuwa na unyoofu katika uhusiano wake na Mungu. Kitabu hiki kinaonyesha kwamba Mungu huwapa thawabu wale walio na imani kwake. (Ebr. 11:6) Inaonyesha kwamba Mungu anatosha, juu ya vitu vingine vyote. Ayubu anarejeshewa kila kitu mwishowe na rafiki zake wanahukumiwa. Tumia kile unachokitaka hapo chini.

Inawezekana Ayubu aliishi kati ya karne ya 18 hadi ile ya 12 K.K. wengi wanaamini aliishi Edomu. Ayubu alishindana na haki ya Mungu. Tunatambua kile ambacho hakukijua: kuna nguvu za kiroho katika mbingu ambazo hutuathiri sisi.

Changamoto ya Shetani kwa Mungu kumjaribu Ayubu kwa kutumia mazingira yake. (Sr. 1-2)

Ayubu anateseka si kwa kile kinachotokea tu, lakini kupitia maswali anayoulizwa na wanafamilia na marafiki na shutuma zao kuhusu yeye kutenda dhambi. (Sr. 3-38)

Ayubu anamhoji Mungu. Mungu anajibu kwa kumpa Ayubu changamoto. Ayubu anakuwa kimya kwanza na kisha mtii. (Sr. 38-42:6) Sababu za Mungu kuhusiana na matukio hazifahamiki wakati wote, lakini watu bado wanaweza kuchagua imani.

Bwana anamthibitisha, anamtetea, na kumrejesha Ayubu. Na pia anawakemea rafiki wake Ayubu. (Sr. 42:7-17)

Tambua kwamba maswali ya Ayubu hayakumkasirisha Mungu.

Kipo wapi?

## Mahali fulani kati ya MABABA hadi USHINDI NA KUMILIKI NCHI YA AHADI

# ZABURI (SURA150)

**Muhtasari wa maelezo**: Zaburi kimeandikwa kwa sehemu kubwa wakati wa Daudi, ingawaje kina baadhi ya zaburi za Musa na za makuhani wa kipindi cha baada ya uhamisho. Daudi aliandika 73 kati ya Zaburi zote. Ni kitabu kinachoonyesha hali ya mwanadamu kutoka sifa hadi kukata tamaa, kutoka kuabudu hadi kukasirika, kutoka upendo hadi kukataliwa. Kinachukuwa wigo mpana wa hisia za mwanadamu na kinaweza kutumiwa na mtu katika kutafuta kwake au kumwabudu Mungu. Pia kinaweza kutumiwa na kanisa kuabudu kama mwili.

Kiliandikwa wakati wa utawala wa Mfalme Daudi na baada ya hapo.

Kilitumika katika kipindi chote cha historia ya Israeli, Yuda na Wayahudi.

Bado kinatumiwa na Wakristo na Wayahudi wa zama hizi kwa ajili ya kutafakari na kuabudu.

Zaburi 118 ndiyo katikati ya Biblia. Sura fupi kuliko zote katika Biblia ni Zaburi 117. Sura ndefu kuliko zote ni katika Biblia ni Zaburi 119.

Zaburi ndicho kitabu kirefu kuliko vyote katika Biblia. Kina mlolongo mzima wa hisia na uzoefu wa mwanadamu. Hakiko kwa ajili ya nyakati za Agano la Kale tu, lakini kinazungumza na watu wote katika nyakati zote. Kimejaa theolojia. Tunaona mada zinazorudiwarudiwa katika Biblia yote, kama vile wokovu au ukombozi katika Zb. 3:2,7 na 19:14. Mada nyingine ni imani katika Mungu mmoja, uumbaji na anguko, kuchaguliwa, agano na nyakati za mwisho.

Kitabu cha Zaburi kwa asili ni kitabu cha nyimbo za kidini na huruhusu watu wa Mungu kuabudu. Kinachukua mada na mawazo mengine mengi na kuyafanya wimbo.

Zaburi ziko kinabii. Katika "Zaburi za Masihi," tunaona kuzaliwa, kufa, na huduma ya Yesu ikitabiriwa. Hizi ni Zaburi ya 2, 8, 16, 22, 24 na 110.

Zaburi ni mashairi. Mitindo mbalimbali ya mashairi inatumika. Katika Zaburi 119, sura iliyo ndefu kuliko zote katika Biblia, kila mstari katika kila kifungu kidogo huanza na herufi ya alfabeti ya Kiebrania. Karibu kila mstari una neno ambalo lina maana inayokaribiana na amri au sheria.

Zaburi ziliandikwa na waandishi mbalimbali kwa kipindi cha miaka mingi. Wengi wao wanatambulishwa katika kichwa cha Zaburi zao. Daudi aliandika 73. Wengine ni watoto wa Kora (11), Asafu (12), Sulemani (moja, labda mbili), na Musa (moja). Zaburi nyingine

hazimtambulishi ye yote kama mwandishi wake. Kora na Asafu wanafikiriwa kuwa wa baada ya uhamisho.

Kuna sehemu tano, au vitabu, ambazo hugawa kitabu cha Zaburi. Kwa kifupi, huonyesha:

Kitabi cha 1: Mungu karibu yetu (Sr. 1-41)

Kitabu cha 2: Mungu anayekwenda mbele yetu (Sr. 42-72)

Kitabu cha 3: Mungu anayetuzunguka pande zote (Sr. 73-89)

Kitabu cha 4: Mungu juu yetu (Sr. 90-106)

Kitabu cha 5: Mungu kati yetu (Sr. 107-150). Hizi ni pamoja na Zaburi za Kupanda (Kupaa) (Sr. 120-134). Watu walikuwa wakiziimba hizi walipokuwa wakisafiri kwenda Yerusalemu kwa ajili ya sikukuu kama vile Pasaka.

Aina nyingine inayofahamika ya chombo cha ushairi kilichotumika katika uandishi wa Kiebrania ni usambamba. Chombo hiki ni kimojawapo ambacho hakijapotea katika tafsiri. Ni mara chache sana kukuta vina na mizani kubakia katika tafsiri ya lugha mbalimbali. Kuna aina tatu ya usambamba: wa mneno yenye maana zinazokaribiana, wa maneno ya kinyume na wa maneno ambatani.

Soma Zaburi 103. Unapoisoma utaona mifano hii ya usambamba: usanisi katika mstari wa 7 na 8, kinyume katika mstari wa 6, maana zinazokaribiana mstari wa 11-12.

Usambamba wenye maneno yenye maana zinazokaribiana huhusisha kurudiwa katika sehemu ya pili ya kile ambacho tayari kimeshatamkwa.

Usambamba wa kinyume huonyesha kukinzana katika wazo.

Usambamba wa usanisi huhusisha kukamilishwa au kuelezwa zaidi lile wazo la sehemu ya kwanza katika sehemu ya pili.

<u>Ni wapi kipo?</u>

# UFALME MMOJA na baadhi wakati wa KIPINDI BAADA YA UHAMISHO

*"Kwa washairi wa Kiebrania, Mungu aliwakilisha uhalisia ambao ulikuwa imara zaidi kuliko hisia zao au waangalizi wa historia ya watu wao. Walikamatana mieleka na Mungu kuhusiana na kila kipengele cha maisha yao, na mwisho wa yote ni tendo lile la kukamatana mieleka ndilo lililowapatia imani. njia moja ya kukiendea kitabu cha Zaburi ni kwa kukifikiria kama ni mkusanyiko wa barua za binafsi ambazo, zikiwekwa pamoja, hudhihirisha picha ya mfululizo wa matukio ya ubinadamu ukipigana mieleka na Mungu."*

*Mungu anataka tuonyeshe hisia zetu za ndani zaidi kwake, sio kujifanya kitu fulani ambacho sivyo tulivyo. "Mashaka, wazimu, kizunguzungu, duni, shangwe, chuki, furaha, kutaka kulipa kisasi, usaliti—unaweza kuyaona haya yote katika Zaburi. Kuchemshwa kwa hisia kwa jinsi hii,*

*ambako wakati fulani nilikuona kama vurugu isiyo na matumaini, sasa naiona kama ishara ya afya. Kutoka katika Zaburi nimejifunza kwamba ninaweza kwa halali kabisa kuleta kwa Mungu chochote kile ninachojisikia kuhusu yeye. Sihitaji kufunika kushindwa kwangu na kujaribu kusafishwa uozo wangu mwenyewe; ni bora zaidi kuyaleta hayo madhaifu kwa Mungu, yeye pekee anayo nguvu ya kuponya."*

Kutoka "The Bible Jesus Read" na Philip Yancey, Haki miliki 2002

# MITHALI (SURA 31)

**Muhtasari wa Maelezo: Mada ya Mithali ni kumcha Bwana na hutoa ushauri wa kimatendo wa namna ya kuishi maisha ya kiungu. Kwa sehemu kubwa kimeandikwa na Sulemani. Baadhi ya mithali huonyesha kutofautiana, baadhi huonyesha mawazo yanayofanana.**

Kiliandikwa kwa sehemu kubwa wakati wa karne ya 10 K.K. na Sulemani na wengine.

Baadhi ya mithali ziliongezwa wakati wa kipindi cha Hezekia (Aguri na Lemueli), karne ya 7 K.K.

Hekima yenye misingi katika kumcha Bwana ndiyo mada: angalia 1:7, 9:10

Hekima ya ki-baba ya Sulemani iko katika sura 1-9. (Sr. 1:8, 5:1) Iangalie katika mistari mingi.

Mithali za kiujumla za Sulemani ziko sura 10-22. (Kimatendo, yaani 11:17, 12:1)

Misemo ya wenye hekima iko katika sura 22-34.

Mithali za Sulemani alizozikusanya Hezekia ziko katika sura 25-29.

Misemo ya Mfalme Aguri, sura 30

Misemo ya Mfalme Lemueli, sura 31:1-9

Uzuri wa mwanamke, sura 31:10-31.

<u>Kipo wapi?</u>

UFALME MMOJA

# MHUBIRI NA WIMBO ULIO BORA

Vyote viwili viliandikwa na Sulemani

# MHUBIRI (SURA 12)

**Muhtasari wa Maelezo:** Mhubiri ni mtazamo wa mwanadamu kuhusu maisha na huonyesha kwamba mwanadamu ana tumaini dogo ambalo kwalo anaweza kutegemea katika wakati ujao (bila ya Mungu). Sulemani anatoa mifano mingi ya hili na kwa ujumla anasema "yote ni ubatili" au hakuna faida. Mwandishi mara kwa mara huonesha njia za Mungu za jinsi ya kufanya vitu. Hili halileti tumaini pekee lakini huzingatia mtazamo wa Mungu kwenye Maisha. Hitimisho lake ni "kumcha Bwana na kuzishika amri Zake" (12:13). Hili hutupa tumaini ambalo watu wote huhitaji.

Mhubiri huonyesha mtazamo wa mwanadamu juu ya kutokufanikiwa kwa mwanadamu duniani na kwamba kutafuta mambo ya kidunia, chakusikitisha ni kwamba, kutatupeleka katika hali ya kukatisha tamaa kabisa. Ubatili (hali ya kutokuwa na maana) mara nyingi inatumika kuelezea vitu kama vile dunia ya asili, anasa, ufanikishaji, jitihada, na hata hekima.

Sura ya 3 inafahamika kwa "Kwa kila jambo kuna majira yake."

Maisha chini ya jua ni ubatili kwa sababu ya udhalimu, ulafi, hekima ya dunia (Sr. 5:8-7:24)

Tatizo hasa ni dhambi (Sr. 7:25-29)

Maisha zaidi chini ya jua katika Sr. 8:1-12:7. Jinsi yalivyo batili katika maeneo mengine.

Hitimisho: Sr. 12: 3-14 "Mche Mungu nawe uzishike amri zake, Maana kwa ujumla ndiyo impasayo mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au baya."

# WIMBO ULIO BORA (SURA 8)

**Muhtasari wa Maelezo:** Wengi wanakubali kwamba haya ni mashairi ya hisia za kupenda yaliyonenwa kati ya mchungaji wa kondoo wa kiume na mchungaji kondoo wa kike. Wanazuoni wengine wanaamini, siku za karibuni, kwamba kusudi la kitabu hiki ni kuonyesha kwamba watu wa Mungu wanaweza kumheshimu Mungu kwa kujamiiana na wenzi wao wa ndoa tu.

Ndoa ni zawadi kutoka kwa Mungu na misingi yake lazima iwe katika uaminifu na kujitoa. Hili hutoa uhuru ndani ya hilo agano kufurahiana.

Wapenzi hutamaniana (Sr.1:2-2:17)

Ndoto za mchungaji wa kike (Sr. 3:1-6:3)

Tamaa ya wapenzi (Sr. 6:4-8:4)

Wapenzi huungana katika ndoa (Sr. 8:5-14)

<u>Ni wapi wapo?</u>

UFALME MMOJA

-----------------------------------------------------------------

# KIFUATACHO: MANABII

*"Ni kwa nini uwasome manabii (wote 17)? Kuna sababu moja ya kuvutia sana: ili umjue Mungu. Manabii ni wahusika wa Biblia walio ufunua Uungu kwa namna ya mguso wenye nguvu zaidi… Yule anayesoma manabii anakutana na sio... uungu uliombali bali Nafsi halisi, Mungu mwenye shauku kama mtu mwingine ye yote ambaye umewahi kukutana naye. Mungu anasikia furaha, na kukatishwa tamaa, na hasira. Analia na kupiga kite kwa maumivu… Manabii hutamka kwa sauti iliyowazi vile Mungu anavyojisikia; Anatupenda."*

"The Bible Jesus Read" na Philip Yancey

Kwenye mtiririko wa Biblia, vipo hivi:

MANABII WAKUU 5=Isaya, Yeremia, Maombolezo, Ezekieli na Danieli.

MANABII WADOGO 12=Hosea, Yoeli, Amosi, Obadia, Yona, Mika, Nahumu, Habakuki, Sefania, Hagai, Zekaria na Malaki.

*(Tafadhali mtiririko huu ili uweze kujua utavipata wapi kwenye Biblia)*

---

# KWA SASA TUNAENDA KUJIFUNZA AU KUVIWEKA VITABU HIVI KWENYE MPANGILIO WA WAKATI.

**(Hili linamaanisha kuviweka kwenye mpangilio wa wakati vilipoandikwa au kutokea, ili tuweze kuvielewa Zaidi kimantiki)**

# YOELI (SURA 3)

**Kiliandikwa kati ya mwaka 835 na 800 K.K au mwaka 430 K.K**

**Muhtasari wa Maelezo:** Yoeli anaonya juu ya hukumu itakayokuja. Anawataka watu watubu na kureje kwa Mungu.

Hadhira ya Yoeli ilikuwa ni taifa la Israeli/Ufalme wa Kaskazini au inawezekana ulikuwa wakati wa uhamisho

Yoeli anaona uharibifu unaokuja. Huzungumzia kuhusu "siku ya Bwana iliyo kuu na ya kutisha" lakini pia tumaini la urejesho (Sura. 2:12-14) Anatumia mfano wa nzige ambao hula nchi, kama mfano wa kuja kwa jeshi litakaloharibu kila kitu.

Mada nyinginezo ni toba, ya kuwa Bwana yuko katikati yao, na vyote huja pamoja katika ile ahadi ya kumwagwa kwa Roho. (Sr. 2:28-29; pia angalia Matendo ya Mitume 2:17)

Kipo wapi?

AMA KIPINDI CHA UFALME ULIOGAWANYIKA/ISRAELI AU BAADA YA UHAMISHO

(Wanazuoni wanatofautiana tarehe ya kuandikwa)

# YONA (SURA 4)

**Muhtasari wa Maelezo:** Kitabu kinaeleza hadithi ya Yona na jinsi alivyomkimbia Mungu. Alipewa nafasi nyingine na alienda Ninawi ambapo aliwaonya watu juu ya hukumu ya Mungu. Walitubu na kumrudia Mungu, japokuwa hili halikumpendeza Yona.

Hakuna ajuaye kwa hakika ni lini kiliandikwa, ni kama kati ya mwaka 782 hadi 753 K.K.

Yona ambaye alikuwa nabii kwa Israeli (Ufalme wa Kaskazini) aliambiwa kuionya Ninawi juu ya ghadhabu ya Mungu. Anakimbia na kwenda Tarshishi kwa merikebu, anamezwa na samaki mkubwa, lakini anaishi. Anapewa nafasi ya pili kwenda Ninawi. Anawahubiria na wanatubu ingawaje Yona hana furaha juu ya hilo.  Inaonyesha kwamba wokovu ni kwa ajili ya watu wote na inaonyesha neema ya Mungu. Yona 3:4 ndio ujumbe wake.

Kipo wapi?

KIPINDI CHA UFALME ULIOGAWANYIKA WA ISRAELI

# AMOSI (SURA 9)

**Muhtasari wa Maelezo:** Amos aliwaonya Israeli kuhusiana na ujio wa maangamizi kutokana na wao kuabudu sanamu, kuridhika mno na kuwatesa maskini.

Alitabiri kwa Ufalme wa Kaskazini kati ya 792 na 740 K.K.

Israeli ilikuwa katika kipindi cha kuona mafanikio na wakadhani kwamba walikuwa wanaendea kipindi kingine cha enzi ya dhahabu chini ya Yeroboamu II. Hata hivyo, hii ilikuwa ni kwa gharama ya walio maskini. (Sr. 4) Amosi aliwaambia ya kuwa walikuwa katika ukingo wa hukumu ya Mungu ambayo ingewatokea muda mchache ujao. (Ilitokea mwaka 722 K.K.) Mungu angeliihukumu Israeli kwa kuridhika kwake kulikozidi kiasi, ibada ya sanamu, na kuwatesa maskini. "Ujiweke tayari kuonana na Mungu wako, Ee Israeli." (Sr. 4:12)

<u>Kipo wapi?</u>

UFALME ULIOGAWANYIKA/ISRAELI

*Nimeona manabii ya kuwa wao ni waandishi wa "kisasa" kuliko ambavyo ungeweza kufikiri. Katika sura hadi sura wanashughulika na mada zile zile ambazo huelea kama wingu juu ya karne yetu: ukimya wa Mungu, kutofautiana kiuchumi, udhalimu, vita, ile hali ya uovu kuonekana kana kwamba unatawala, mateso yanayoathiri dunia yetu ambayo hayajadhihirishwa. Hizi, mada zile zile ambazo huonekana katika maeneo fulani fulani ya Ayubu, Zaburi, Mhubiri, na pia Kumbukumbu la Torati, manabii huzileta katika muonekano au mtazamo wa karibu sana, kana kwamba wanaangalia kwa kutumia hadubini.*

"The Bible Jesus Read" na Philip Yancey

# HOSEA (SURA14)

**Muhtasari wa Maelezo:** Hosea anasimulia Upendo wa Mungu na msamaha wake kwa watu wenye dhambi kwa njia tofauti tofauti, ikiwa ni pamoja na mahusiano ya mume na mke.

Kiliandikwa kwa Israeli kati ya 755 na 725 K.K. Ni picha ya ndoa iliyovunjika, ukombozi, na msamaha. Mara nyingi imefikiriwa kuwakilisha ndoa ya Mungu kwa Israeli. (Sr. 1-3:5)

Mungu anaishutumu Israeli kwa unafiki na anawasihi, mlinganisho wa kile ambacho Israeli wanafanana nacho…ina maana Sr. 7…tanuru, keki, hua. Wakati wakiabudu miungu ambayo imetengenezwa na wanadamu, Hosea anawaambia kwamba wanalikataa tumaini pekee walilonalo. (Sr. 4-14)

<u>Kipo wapi?</u>

UFALME ULIOGAWANYIKA/ISRAELI

# MIKA (SURA 7)

**Muhtasari wa maelezo:** Onyo la hukumu ya Mung una msamaha kwa wale ambao watatubu

Ilitokea kati yam waka 750 hadi 687 K.K., alitabiri zaidi kwa Ufalme wa Kaskazini

Alibashiri kuanguka kwa Samaria, ambayo ni mji mkuu wa Israeli, na hali ya kuhuzunisha isiyoepukika ya Israeli. Pia alibashiri utawala ujao wa ki-Mungu wa Yerusalemu na urejesho wa watu Wake.

Mistari inayojulikana ni Mika 5:2 na 6:8

--------------------------------------------------------------------------------

# MWANZO WA MANABII WALIOZUNGUMZIA YUDA

# ISAYA (SURA 66)

**Muhtasari wa Maelezo:** Isaya anawaita Yuda wamrudie Mung una kuwaeleza wokovu wa Mungu kupitia Masihi. (mwaka 740 hadi 681)

Isaya kinafikiriwa kuwa kama Biblia ndogo. Kina sura 66. Biblia ina vitabu 66. Wengine wanasema unaweza kuwepo uhusiano kati ya Isaya na Agano la Kale na Jipya.

Sura 39 za kwanza katika Isaya (huwakilisha AK) kwa ujumla zinahusu hukumu (ingawaje kuna neema kiasi). Inaonekana zimejikita zaidi kwenye agano la kale na tumaini kiasi tu (kama Agano la Kale). Sura 27 zinazofuata (40-66) vinahusiana na faraja na tumaini ambazo kwa sehemu kubwa ni kama AJ. (Kuna vita 27 katika AJ.) Utukufu wa Mungu na mistari ya kinabii kuhusiana na Masihi imetolewa katika sehemu hii. Isaya alitumika kipindi cha wafalme watano kwa kama miaka 60. Tumia mengine zaidi kutoka hapo chini.

Alitumika kutoka 740 K.K. hadi 681 K.K. chini ya wafalme watano, kuanzia Uzia na kuishia na Manase.

Alitabiri kwa Israeli na Yuda. Alitabiri kuhusu mataifa yaliyowazunguka.

Utabiri wa Masihi (Sr. 53). Baadhi bado yanatarajiwa kutokea! (Sr. 60-66)

Dhambi za Yuda zinakabiliwa na kushutumiwa. (Sr. 1-5)

Mungu anatoa kwa Yuda na Israel wakati mpya ujao kwa neema na hukumu. (Sr. 6-12)

Mungu atatoa hukumu na neema kwa dunia. (Sr.13-27)

Neno lililotamkwa na Mungu linatolewa kwa dunia. (Sr. 28-35)

Mpito… “Ni nani utamtegemea?” (Sr. 36-39)

Mungu atawapatia faraja mateka. (Sr. 40-55)

Kutakuwa na Utukufu hapo baadae! (Sr. 56-66)

<u>Ni wapi kipo?</u>

UFALME ULIOGAWANYIKA HASA YUDA PEKE YAKE

# YEREMIA na MAOMBOLEZO

**Muhtasari wa Maelezo kwa vitabu vyote:** Ilitukia kati yam waka 626 hadi 586 K.K. Yeremia alihudumu Yuda chini ya wafalme watano, Yosia hadi Zedekia. Anajulikana kama Nabii wa machozi/ nabii aliaye, lakini alikuwa shupavu, nabii mwenye uvumilivu, ambaye mara nyingi alitumia mifano. Alionya juu ya uharibifu utakaofanywa na Babeli na aliwataka Yuda wamrudie Mungu. Maombolezo hutimiza laana ya kumbukumbu la Torati 28.

Yeremia alihudumu Yuda chini ya wafalme watano, Yosia hadi Zedekia kuanzia 626 hadi 586 K.K.

Anajulikana kama nabii mwombolezaji, alikuwa nabii imara, mwenye uvumilivu aliyetumia mara nyingi lugha ya ishara.

Alionya juu ya kuharibiwa kwa Babeli, aliwataka Yuda kumrudia Mungu.

Maombolezo hutimiza laana za Kumbukumbu la Torati 28

# YEREMIA (SURA 52)

Kwa ujumla, kitabu kinakazia hukumu ya Mungu juu ya kukosa uaminifu kwa Yuda na wale ambao wangekuwa ndio watu wa kulitunza agano. Mungu pia anataka watu hawa siku moja waje kulijua agano jipya. Watu wengine wanamwita Yeremia nabii anayeomboleza lakini anaonyesha kwamba yeye yuko imara kama misumari. Mtu huyu, licha ya kuteseka sana, anaendelea kutoa Neno la Mungu, licha ya hili kuathiri mazingira.

Yeremia aliwekwa wakfu na Mungu akiwa tumboni. Ilikuwa ateseke akiwa katika kulinena Neno la Mungu, lakini aliahidiwa ulinzi wa Mungu. (Sr. 1)

Aliishutumu Yuda kwa kuabudu sanamu na imani potofu. (Sr. 2-10)

Alipambana na Mungu na Yuda. (Ch. 11-20)

Aliwakabili wafalme, manabii wengine, na watu kwa sababu ya imani zao potofu (Sr. 21-29)

Alitabiri urejesho wa taifa, nchi ya ahadi, agano jipya, kuheshimiwa kwa agano la Daudi. (Sr. 30-33)

Aliihukumu Yuda na uasi wake dhidi ya Babeli na Mungu (Sr. 34-45)

Mungu alinena kupitia Yeremia kuhusiana na hukumu ya mataifa mengine (Sr. 46-51)

Hatimaye, alisema kuhusiana na anguko la Yerusalemu, kuharibiwa kwa hekalu na uhamisho wa watu wake, lakini bado, kuendelezwa kwa agano la Daudi. (Sr. 52)

## MAOMBOLEZO (SURA 5)

Ikiwa Yeremia ndiye mwandishi, (na yaelekea kuwa ndivyo) huenda kiliandikwa mnamo 587 hadi 580 K.K.

Huonyesha uharibifu ambao ulitokea Yerusalemu wakati ikiwa imezingirwa na Babeli kwa muda wa miaka miwili. Mengi ya mateso hayo yalitabiriwa katika Kumbukumbu la Torati 28 ambalo hutupa zile laana za kutotii.

Hata hivyo wakati wa mateso, uaminifu wa Mungu unaweza kuonekana, na urejesho unawezekana. (3:22-24)

<u>Kipo wapi?</u>

UFALME ULIOGAWANYIKA

## NAHUMU (SURA 3)

**Muhtasari wa Maelezo:** Alitabiri kuangamizwa kwa Ninawi. Sura tatu zinatupa ufafanuzi wa kina kwanini na kwa jinsi gani litakavyotokea. Kiliandikwa yapata miaka 100 baada ya Yona.

Kiliandikiwa mataifa mawili ya Yuda na Ninawi. Uharibifu ulitokea mwaka 612 K.K. kiliandikwa baada ya mwaka 660 na kabla ya mwaka 630 K.K

<u>Kipo wapi?</u>

YUDA PEKE YAKE

# HABAKUKI (SURA 3)

Kimeandikwa kati ya 640 hadi 609 K.K.

**Muhtasari wa Maelezo:** kuonesha kwamba Mungu bado anautawala ulimwengu licha ya ushindi wa uovu.

Anamuuliza Mungu kwa nini hafanyi cho chote kuhusiana na uovu wa Yuda. Mungu anasema anawatuma Babeli. Habakuki ni lazima amtegemee Mungu licha ya Mungu kuwatumia Babeli walio waovu na pengine asiuone urejesho wakati wa uhai wake. Kitabu hiki huonyesha kwamba Mungu ndiye mwenye kutawala duniani licha ya uovu.

"Mwenye haki ataishi kwa imani" ilitamkwa kwanza katika Hab. 2:4, na pia 3:17-18

<u>Kipo wapi?</u>

YUDA PEKE YAKE

# ZEFANIA (SURA 3)

**Muhtasari wa Maelezo:** Kuwaambia Yuda wamrudie Mungu na pia kuona kukata tamaa kwao wenyewe.

Kinaelezea baadhi ya nabii kutimia wakati wa utawala wa Yosia, 640-609 K.K., na kiliandikwa mnamo wakati huu.

Hukumu ya Mungu iko juu ya wale watendao dhambi dhidi yake lakini Baraka ni kwa ajili ya wale wanaomfuata. Mungu hana wajukuu. Kila mtu lazima aamue yeye mwenyewe binafsi kwamba Mungu ni nani katika maisha yake.

Unabii wa Mungu uko kinyume na Yuda na hukumu kwa mataifa yanayozunguka inatolewa pia.

Katika sura ya mwisho, Zefania anazungumza kuhusu wakati wa utukufu ujao wa Israeli/Yuda.

<u>Ni wapi vipo?</u>

UFALME ULIOGAWANYIKA/YUDA PEKE YAKE

KIPINDI CHA UHAMISHO

---------------------------------------------------------------------------------------------------------

# EZEKIELI (SURA 48)

Muhtasari wa Maelezo: Alizungumza na Wayahudi wakiwa kwenye nchi yao wakati akiwa utumwani Babeli. Aliwataka wote watubu ili hatimaye wawe na ujasiri.

Kiliandikwa kati yam waka 593 hadi 573 K.K

Ezekieli alichukuliwa kutoka Israeli mwaka 597 K.K. Wakati anaishi Babeli, alinena na Yuda na mataifa yanayoizunguka akiwatangazia hukumu ya Mungu juu yao. Hata hivyo, baadaye anawajulisha juu ya wokovu wa hapo mbeleni wa watu Wake. Anapokea maono na anaona kiti cha enzi cha Bwana.

Kuitwa kuwa mlinzi. (Sr. 1-3)

Yerusalemu na Yuda kuhukumiwa (Sr. 4-24)

Ananena dhidi ya mataifa mengine (Sr. 25-32)

Anasema kuhusu kile kitakachotokea baada ya anguko la Yerusalemu. Anabainisha mengi kuhusu wakati ujao wa Israeli. (Sr. 33-39)

Anapata maono ya urejesho, hasa wa lile hekalu. (Sr. 40-48)

Kipo wapi?

## KIPINDI CHA UHAMISHO

# DANIELI (SURA12)

Muhtasari wa Maelezo: Wasikilizaji wake ni watumwa wenzake waliokuwa Babeli. Alitolea maelezo ya nini kitakachotokea kwa Wayahudi waaminifu huko. Aliwaonesha pia ni jinsi gani Mungu anatawala mbingu na Dunia, mwelekeo wa taifa, nguvu ya asili na jinsi gani anavyowajali watu wake.

Kiliandikwa kati ya mwaka 605 hadi 536

Alichukuliwa kutoka Israeli akiwa kijana mwaka 605 K.K. na aliishi Babeli maisha yake yote yaliyofuata.

Alipokuwa na miaka kama 85, aligundua, baada ya kusoma Yeremia, kwamba ilikuwa ndio wakati wa baadhi ya mateka kurudi kwao. (Angalia Yeremia Sura 25 na 29 na Daniel 9:1-2)

Sura 6 na kwanza za Danieli zina zile simulizi ambazo zinatambulika sana kwa kawaida:

Vijana wanakuwa waaminifu kwa Mungu, hasa hasa chakula wanachokula (Sr.1)
Ndoto ya mfalme Nebukadrezana tafsiri (Sr.2)
Sanamu ya dhahabu na tanuru ya moto (Sr. 3)

Nebukadreza na ukichaa (Sr. 4)
Kiganja kikiandika ukutani (Sr. 5)
Danieli katika tundu la Simba (Sr. 6)

Ikiwa unataka kuongeza yaliyo hapo chini, fanya hivyo. Inaweza kusemwa kwamba sura sita za mwisho huzungumza kuhusu kile kinachotokea kuhusiana na Ufalme wa Mungu (Sura ya 7) na falme za dunia…Wamedi/Waajemi, Wayunani, na Warumi. Angalia hapo chini.

Sura 6 za mwisho ni maono ya Danieli:
Wanyama wakubwa wanne na mahakama ya mbinguni (Sr. 7)
Maono ya kondoo dume, mbuzi na pembe (Sr. 8)
Maono ya maombi ya Danieli na majibu yake (Sr. 9)
Maono ya mgogoro wa mwisho (Sr. 10-12)

Kipo wapi?

KIPINDI CHA UHAMISHO

# OBADIA (SURA 1)

Muhtasari wa Maelezo: Pengine kiliandikwa kati ya 586 na 553 K.K. Pengine yalitokea mwaka 585 K.K. Kilitabiri uharibifu wa Edomu ambayo ilikuwa kusini magharibi ya Israeli/Yuda na ilikuwa adui wa Yuda.

Kiliandikwa kuonesha kwamba Mungu huwahukumu wale ambao huwatesa watu wake.Uharibifu wa Edomu ulitokana na kuendelea kwa unyanyasaji wa Yuda na walifurahia uharibifu uliofanywa na Wababeli.

Kipo wapi?

YUDA PEKE YAKE

---

## Mwanzo wa kipindi cha baada ya uhamisho

# HAGAI (SURA 2)

**Muhtasari wa Maelezo:** Kuwaita waliorudi toka utumwani kulikamilisha hekalu.

Hiki kiliandikwa mnamo 520 K.K. na kiliwahamasisha wale waliorudi kutoka uhamishoni kuanza kulijenga tena hekalu. Hatimaye mwaka 515 K.K. lilikamilika. Hagai alikuwa amekwisha kuliona hekalu la Sulemani, kwa hiyo yeye alikuwa mzee zaidi kati ya hao waliorudi.

Kipo wapi?

## KIPINDI BAADA YA UHAMISHO

*Katika "The Bible Jesus Read," Philip Yancey anatoa dondoo kadhaa za kuwasoma manabii. Anatoa maeneo matatu ya kusaidia kushinda vikwazo vya kusoma vitabu vya manabii na kusadia kugundua ujumbe wa msingi wa kitabu.*

*(1) "Sasa" nabii kimsingi zinahusiana na mambo yanayohusu wakati aliokuwepo nabii mwenyewe.*

*(2) "Baadaye" nabii zinaondolewa kutoka katika wakati wa maisha ya kila nabii mwenyewe, lakini baadaye zinatimia katika historia.*

*(3) "Baadaye zaidi" nabii zina hali ile ya kuendelee kubaki katika wakati ujao.*

# ZEKARIA (SURA14)

Muhtasari wa Maelezo: Aliwatia moyo watu warudi kulijenga hekalu. Pia aliwaonesha ukombozi utakaokuja baadaye utakaoletwa na Masihi.

Uwezekano mkubwa 520 K.K. Alikuwa wa wakati mmoja na Hagai. Aliwahamasisha waliorudi kutoka uhamishoni kulijenga upya hekalu.

Yeye pia alipata maono wakati wa usiku mara nane, mengine yalihusu nyakati zetu za mwisho, (mada za nyakati za mwisho).

Sura tano za mwisho zinahusisha nabii kuhusu kuja kwa Bwana mara ya kwanza na ya pili (mengine kama Mchungaji).

Kipo wapi?

## KIPINDI BAADA YA UHAMISHO

# MALAKI (SURA 4)

**Muhtasari wa Maelezo:** Aliwakabili wat una dhambi zao na kuwataka warejee kwa Mungu.

Mnamo 438-433 K.K. Alionya dhidi ya dhambi ya Wayahudi na makuhani wakati wa safari ya pili ya Nehemia.

Anazungumza kuhusu mambo kama kukosa uaminifu, kumwibia Mungu, na Siku ya Bwana. Alitumia maswali sita ili kuyapa sura mambo yaliyopingana na mtazamo uliokuwepo.

Kipo wapi?

KIPINDI BAADA YA UHAMISHO

---

## *MAELEZO YA JUMLA KUHUSU KITABU KILIPO*

**Katikati ya kipindi cha MABABA na USHINDI NA KUMILIKI NCHI**

Ayubu

**UFALME MMOJA**

Zaburi

Mithali

Mhubiri

Wimbo Ulio Bora

**UFALME ULIOGAWANYIKA**

Isaya (wote Israeli na Yuda)

Hosea (wote Israeli)

Amosi (wote Israeli)

Yona (wote Israeli)

Mika (wote Israeli)

**YUDA PEKE YAKE** (Hili ni baada ya Israeli kwenda utumwani mwaka 722 K.K.)

Isaya

Yeremia

Maombolezo

Habakuki

Zefania

Nahumu

**KIPINDI CHA UHAMISHONI**

Yoeli (?)

Obadia

Ezekieli

Danieli

**KIPINDI BAADA YA UHAMISHO**

Baadhi ya Zaburi (upandaji)

Hagai


Zechariah

Malachi

# RAMANI




Ramani ya 1 Dunia ya Agano la Kale



Ramani ya 2 Ushindi na Kuimiliki nchi





Ramani ya 3 Ufalme Mmoja





Ramani ya 4 Ufalme Uliogawanyika




Ramani ya 5 Kipindi cha Uhamisho




Ramani ya 6 Kipindi Baada ya Uhamisho




Ramani ya 7 Mashariki ya Kati ya Sasa